



Kulikuwa na  
mwanamme mrefu  
sana.

Jembe lake lilikuwa  
fupi mno.



Mlango wake  
ulikuwa chini mno.



Kitanda chake  
kilikuwa kifupi mno.



Baisikeli yake  
ilikuwa fupi mno.



Mtu huyu alikuwa  
mrefu zaidi ya  
vifaa vyote.




Aliamua  
kurekebisha vifaa  
vyake.


Aliutengeneza mpini  
wa jembe mrefu  
sana.



Akazitengeneza  
fremu refu za  
mlango.




Akakitengeneza  
kitanda kirefu sana.



Kisha akainunua  
baiskikeli iliyokuwa  
refu mno.

Akaketi juu ya kit  
kilichokuwa juu  
sana. Akala kwa  
kutumia uma  
iliyokuwa refu mno.





Aliamua kuhamia  
katika msitu  
mkubwa. Akaishi  
kwa miaka mingi.

